

Sheria (1982:316) *inayoharamisha ukeketaji wa kijinsia wa wanawake*

---

# INFORMATION OM KÖNSSTYMPNING

*Swahili*



Sweden

# Ukeketaji wa kijinsia

**Ukeketaji wa kijinsia hauruhusiwi  
Sweden kulingana na sheria ya Kiswidi  
(SFS 1982:316).**

Yoyote ambaye anakiuka sheria hii anaweza kuhukumiwa hadi miaka 10 gerezani, hata ikiwa ukeketaji wa kijinsia unatokea nje ya Sweden. Majaribio na matayarisho ya ukeketaji wa kijinsia ni kinyume cha sheria, na pia kumshawishi mtu mwingine kufanya ukeketaji wa kijinsia. Pia ni kinyume cha sheria kutoripoti jambo ikiwa unajua kuwa ukeketaji wa kijinsia utafanywa. Mbali na yule anayefanya ukeketaji wa kijinsia haswa, wazazi wa msichana wana jukumu la kuzuia ukeketaji wa kijinsia kutokea na wanaweza kufungwa kwa hatia hiyo nchini Sweden.

*Sheria (1982:316) inayoharamisha  
ukeketaji wa kijinsia wa wanawake*



LÄNSSTYRELSEN  
ÖSTERGÖTLAND



**Polisen**

# Athari

**Ukeketaji wa kijinsia wa wanawake, pia unaojulikana kama tohara ya wanawake, ni unyanyasaji unaolengwa kwa kubadilisha au kuharibu viungo vya kijinsia vya nje vya msichana au mwanamke. Ukeketaji wa kijinsia unasababisha madhara kwa njia nyingi, na unaweza kusababisha shida zifuatazo hapohapo na baadaye maishani:**

- Utokaji damu mkuu wakati wa taratibu
- Maambukizi
- Maumivu kwenye eneo la kijinsia
- Shida kukojoa
- Matatizo wakati wa hedhi
- Maumivu wakati wa ngono, kwa mwanamke na mwanamume
- Uharibifu unaoweza kumzuia mwanamke kuweza kupata mimba
- Matatizo ya kuzaa
- Shida za kiakili
- Kifo

# **Aina ya ukeketaji wa kijinsia**

**WHO inafafanua aina nne za ukeketaji wa  
kijinsia:**

**Aina 1:** Klitorisi na/au funiko la klitorisi linaondolewa.

**Aina 2:** Klitorisi, midomo ya ndani (labia ya ndani) na mara nyingine midomo ya nje (labia ya nje) inakatwa.

**Aina 3:** Klitorisi, midomo ya ndani (labia ya ndani) na midomo ya nje (labia ya nje) inakatwa na kushonwa pamoja kufunika shimo la uke.

**Aina 4:** Taratibu zote zingine ambazo zinaharibu viungo vya kijinsia kama vile kuchanja.

”Sunnah” mara nyingine inatajwa wakati kunazungumzwa kuhusu aina tofauti za ukeketaji wa kijinsia. Aina zote za ukeketaji wa kijinsia, zikiwemo zinazoitwa “sunnah”, ni kinyume cha sheria!





# Polisen



LÄNSSTYRELSEN  
ÖSTERGÖTLAND

*Sheria (1982:316) inayoharamisha ukeketaji wa kijinsia wa wanawake*

*Detta material är framtaget av Länsstyrelsen Östergötland.*